# MFUKO WA ELIMU

www.tea.or.tz Toleo la 4 Julai - Septemba 2024







## WANAFUNZI 400 WAPATA HUDUMA ZA MABWENI KUPITIA UFADHILI WA TEA...*Uk.01*

Mbunge wa Manyoni atambua kazi nzuri ya TEA...*uk.08*

TEA na TotalEnergies zatoa madawati 130 wilayani Kibiti...*uk.04*

*“Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu ya Elimu”*

# KUHUSU TEA

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya 2001 chini ya kifungu cha 5 (1) ili kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu, ulioanzishwa kwa sheria hiyo hiyo. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

Madhumuni ya Mfuko wa Elimu ni kuongeza nguvu za Serikali katika kugharamia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa, katika ngazi zote za Elimu kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.

## MFUKO WA ELIMU

Mfuko wa Elimu unapokea rasilimali fedha na vifaa ambazo hukusanywa na kuratibiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa lengo la kufadhili miradi ya elimu nchini kutoka vyanzo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

TEA imepewa jukumu la kuhamasisha wadau mbalimbali nchini na nchi za nje kuchangia rasilimali mbali mbali kwa lengo la kusaidia juhudi za Serikali kuinua ubora, na kuongeza upatikanaji wa elimu kwa usawa.



## Dira

Kuwa Mfuko wa Elimu bora, wenye hadhi ya kimataifa, unaotatua changamoto za elimu nchini, kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika kuchangia maendeleo endelevu nchini.



## Dhamira

Kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuzigawa rasilimali hizo kwa ufanisi ili kufadhili miradi ya elimu ili kuboresha upatikanaji wa elimu bora kwa usawa.

# YALIYOMO

Kuhusu TEA....................................................i

Salaam za Mkurugenzi Mkuu......................ii

Wanafunzi 400 Wapata Huduma za Mabweni Kupitia Ufadhili wa TEA...........01

Mfuko wa Elimu wa Taifa Wakamilisha Ujenzi wa Nyumba Sita za Walimu Kisarawe.........................................................02

TEA na TotalEnergies Zatoa Madawati 130 Wilayani Kibiti.....................................04

Habari Picha.................................................05

Mbunge wa Manyoni Atambua Kazi Nzuri ya TEA...............................................08

TEA na EATV Zafanya Matembezi Kuhamasisha Kampeni ya 'Namthamini'................................................09

TEA, SAUT Wazungumza Maendeleo Sekta ya Elimu.............................................11

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Gesibora Wateta jijini Dodma..................12

**BODI YA WAHARIRI:**

**Mwenyekiti**
Masozi Nyirenda

**Mhariri**
Bestina Magutu

**Wachangiaji**
Eliafile Solla
Joyce Minja

**ANUANI:**

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),
S.L.P 2516,
**Dodoma - Tanzania.**

Tovuti: www.tea.or.tz
Barua pepe: info@tea.or.tz



**Dkt. Erasmus F. Kipesha**
*Mkurugenzi Mkuu - TEA*

# SALAAM ZA MKURUGENZI MKUU

Karibuni kwenye Jarida la Nne (4) la Mfuko wa Elimu. Katika toleo hili, tunapitia baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025, kuanzia Julai hadi Septemba 2024. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kukamilika kwa ujenzi wa mabweni kwa wanafunzi wa kike 400 katika mikoa ya Pwani na Lindi. Hatua hii imeleta mazingira salama na rafiki zaidi kwa ajili ya kujifunza, huku ikipunguza changamoto ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shuleni kila siku. Hali hii pia imeongeza mahudhurio na kupunguza hatari ya unyanyasaji na mimba za utotoni.

Pia katika robo hii, tumeshuhudia kukamilika kwa ujenzi wa nyumba sita za walimu kupitia ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa (TEA) huko Kisarawe, Mkoani Pwani. Walimu ni nguzo muhimu katika mfumo wa elimu hivyo ili kuwa na makazi bora na salama karibu na shule, TEA inahakikisha kuwa walimu wanapata mazingira yanayowasaidia kujiandaa vyema na kuzingatia majukumu yao ya kufundisha.

Aidha katika robo hii, TEA kwa kushirikiana na TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd ilifanikiwa kutoa madawati 130 kwa shule za Rufiji. Ushirikiano huu unaonyesha jinsi sekta ya umma na binafsi inavyoweza kushirikiana kwa ufanisi katika kushughulikia changamoto za rasilimali katika sekta ya elimu.

Kwa upande mwingine, TEA na EATV waliongoza matembezi ya hisani kufanikisha kampeni ya "Namthamini" inayolenga kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa kike. Kampeni hii inalenga zaidi afya na usafi, kwa kuhakikisha upatikanaji wa taulo za kike na maji safi.

Kwa kumalizia, ni wazi kuwa miradi ya TEA inaendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha miundombinu ya elimu, hivyo kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Ushirikiano kati ya wadau wa elimu, ikiwemo sekta binafsi, ni muhimu katika kuhakikisha maendeleo endelevu kwenye sekta ya elimu.

# WANAFUNZI 400 WAPATA HUDUMA ZA MABWENI KUPITIA UFADHILI WA TEA

Pwani na Lindi





*Moja kati ya Mabweni katika Shule ya Sekondari Rafsanjani iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani ambayo ujenzi wake umefadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).*

Wanafunzi wa kike 400 kutoka mikoa ya Pwani na Lindi wamepata huduma ya mabweni kupitia ufadhili wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), ambayo imefadhili ujenzi wa mabweni matano katika shule tatu za mikoa hiyo. Jumla ya Sh. Milioni 534.06 zilitumika kugharamia miradi hiyo.

Shule ya Sekondari Kwala wilayani Chalinze Mkoani Pwani, ilijengewa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 160 kwa gharama ya Sh. milioni 228.07.

***Inaendelea Uk. 03***

# MFUKO WA ELIMU WA TAIFA WAKAMILISHA UJENZI WA NYUMBA SITA ZA WALIMU KISARAWE

Kisarawe

> Tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutambua mchango wa walimu na kuwathamini kwa kuwajengea nyumba hizo kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania
>
> **Bw. Patience Mponda**
> *Mkuu wa Shule ya Sekondari Vikumburu*

Jumla ya **Sh. 185,000,000** kutoka Mfumo wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Eimu Tanzania (TEA) zimetumika kukamilisha ujenzi wa nyumba sita za walimu katika Shule ya Sekondari ya Vikumburu Wilayani Kisarawe Mkoani Pwani.

Kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa mradi huo walimu sita na familia zao sasa wamepata makazi bora katika eneo la shule hali ambayo inawapa fursa nzuri ya kujiandaa na kufundisha wanafunzi wao.

Akizungumza na maafisa wa TEA waliofika shuleni hapo kukagua ukamilishwaji wa mradi huo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Vikumburu, Bw. Patience Mponda alisema walimu sasa wanapata muda wa ziada wa kufundisha wanafunzi kwa vile wanakaa maeneo karibu na shule.

Aidha, Mwalimu Mponda aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutambua mchango wa walimu na kuwathamini kwa kuwajengea nyumba hizo kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania na kuahidi kuwa, upatikanaji wa nyumba hizo utachochea hamasa ya walimu kufundisha kwa bidii na hivyo kuongeza ufaulu wa wanafunzi.



*Moja kati ya nyumba sita za walimu zilizojengwa katika Shule ya Sekondari ya Vikumburu Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani kwa ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa.*

Inatoka Uk. 01

## WANAFUNZI 400 WAPATA HUDUMA YA MABWENI KUPITIA UFADHILI WA TEA



*Moja kati ya Mabweni katika Shule ya Sekondari Kwala iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani ambayo ujenzi wake umefadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).*

Shule ya Sekondari Rafsanjani iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, ilijengewa bweni moja kwa Sh. milioni 120, likiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 80. Aidha, shule ya Sekondari Kikaro iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, ilijengewa mabweni mawili yenye uwezo wa kubeba wanafunzi 160 kwa gharama ya Sh. milioni 189.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kwala, Wilayani Chalinze Mkoani Pwani Bw. Ismailia Ng'ondya amesema ufadhili wa Mfuko wa Elimu katika ujenzi wa mabweni hayo umesaidia kuboresha mahudhurio na kuongeza ufanisi kwa wanafunzi wanufaika.

Akizungumza na maafisa wa TEA waliofika kukagua miradi hiyo, Mwalimu Ng'ondya alisema awali wanafunzi hao walilazimika kutembelea zaidi ya kilometa 16 ili kuhudhruia masomo.

Kwa upande wa Mkuu wa Shule ya Sekondari Kikaro iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze mkoani Pwani, Bw. Emmanuael Kahabi na Mkuu wa Shule ya Sekondari Rafsanjani Bi. Koku Nyimbwa wamesema ufadhili wa Mfuko wa Elimu utawaepusha wanafunzi hao na hatari ya kupata mimba za utotoni zinazotokana na vishawishi wanavyokumbana navyo wakiwa katika mazingira ya nje ya shule.

Walimu hao wametoa shukrani kwa Serikali kwa kutoa fedha za ufadhili wa ujenzi wa mabweni hayo kupitia Mfuko wa Elimu.

# TEA NA TOTALENERGIES ZATOA MADAWATI 130 WILAYANI KIBITI

Kibiti




*Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd Bi. Getrude Mpangile (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa TEA CPA. Mwanahamisi Chambega katika hafla ya kukabidhi madawati katika Shule ya Msingi Jaribuni Mpakani.*

**Miongoni mwa majukumu ya TEA ni kutafuta rasilimali fedha kutoka kwa wadau mbalimbali na kuzigawa katika taasisi za elimu ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia hivyo tunawakumbusha kutunza vifaa hivyo...**

Kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) wamekabidhi madawati 130 katika shule ya Msingi Jaribuni Mpakani na Shule ya Msingi ya Kitundu zote za Wilayani Kibiti Mkoani Pwani ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ushirikiano baina yao katika kuboresha miundombinu ya elimu nchini.

Hafla ya kukabidhi madawati hayo iliongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kibiti Kanali Joseph Kolombo katika Shule ya Msingi Jaribuni Mpakani tarehe 24 Septemba 2024.

Akizungumza katika hafla hiyo Kanali Kolombo ameahidi na kusema, madawati hayo yatatunzwa ili kuendelea kuwanufaisha wanafunzi na kuongeza kuwa Wilaya ya Kibiti imekuwa ikinufaika na miradi kadhaa ya TEA ukiwemo ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Kitundu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd Bi. Getrude Mpangile amesema madawati hayo 130 ni sehemu ya madawati 200 yenye thamani ya Sh. Milioni 25.9 yaliyotolewa na kampuni hiyo kwa shule tatu za Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam.

*Inaendelea Uk. 07*

# HABARI KATIKA PICHA; UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA SHULE YA MSINGI KINYAMALE WILAYANI KIBITI








*Muonekano wa ndani na nje wa chumba cha darasa katika Shule ya Msingi Kinyamale iliyopo Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani. Ujenzi wa Mradi huo umefadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).*

# HABARI KATIKA PICHA; UJENZI WA VYUMBA ZA WALIMU KATIKA MKOA WA LINDI






*Muonekano wa Nyumba nne (4) za walimu katika Shule ya Sekondari Mandare, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi zilizojengwa kwa ufadhili wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).*



*Ujenzi wa nyumba za walimu ukiendelea katika Shule ya Sekondari Ngongo mkoani Lindi ukifadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).*




*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Jaribuni Mpakani wakifuatilia hafla ya kukabidhiwa madawati*




*Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa TEA, CPA. Mwanahamisi Chambega akitoa salaam katika hafla ya kukabidhi madawati katika shule ya Msingi Jaribuni Mpakani.*

*Inatoka Uk. 04*

Kufuatia msaada huo Shule ya Msingi Jaribuni Mpakani imepata madawati 65, Shule ya Msingi Kitundu madawati 65 na Shule ya Msingi Makuburi ya Jijini Dar es Salaam imepata madawati 70.

Bi. Mpangile ameeleza matumaini yake kwamba msaada huo utasaidia kuweka hamasa kwa wanafunzi kujifunza kwa bidii na hivyo kuchangia kukuza ufanisi na ufaulu wa shule zilizonufaika na madawati hayo.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa TEA, CPA Mwanahamisi Chambega amezikumbusha shule zilizonufaika na msaada huo wa madawati kuyatunza vyema ili yawe na manufaa kwa wanafunzi wengi.

“Miongoni mwa majukumu ya TEA ni kutafuta raslimali fedha kutoka kwa wadau mbalimbali na kuzigawa katika taasisi za elimu ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia hivyo tunawakumbusha kutunza vifaa hivo”. Amesema CPA Chambega.

Msaada huo unafuatia mkutano baina ya wawakilishi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd uliofanyika tarehe 27 Agosti 2024 Makao Makuu ya TEA Jijini Dodoma kujadili namna wanavyoweza kushirikiana katika miradi ya kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia hapa nchini.

# MBUNGE WA MANYONI ATAMBUA KAZI NZURI YA TEA

Dodoma

Mbunge wa Manyoni Mashariki Mkoani Singida Mhe. Dkt. Pius Chaya ameipongeza Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia hapa nchini.

Dkt. Chaya amesema, ameshuhudia miradi mingi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, mabweni, nyumba za walimu pamoja na maktaba za Sayansi ambazo zimejengwa na TEA.

Akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus Kipesha tarehe 13 Septemba 2024 katika ofisi za TEA makao makuu zilizoko Ilazo Jijini Dodoma alipofika kwa lengo la kutoa shukrani kwa miradi ya elimu iliyofadhiliwa na Mfuko wa Elimu wa Taifa jimboni kwake ambapo amesema imesaidia katika kuinua ubora wa elimu.

"Jimboni kwangu Manyoni Mashariki ni wanufaika wa miradi inayotekelezwa na TEA hivyo nimekuja kuwashukuru kwa miradi hiyo, amesema Dkt. Chaya."

Ameitaja miradi ya elimu ambayo imefadhiliwa na TEA jimboni Manyoni Mashariki kuwa ni ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari Sasajila, vyumba vitatu vya madarasa Shule ya Msingi Sanza na Kintinku pamoja na matundu 24 ya vyoo Shule ya Msingi Kintinku.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha amemshukuru Mbunge huyo kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa miradi hiyo hadi imekamilika.



*Mbunge wa Manyoni Mashariki Mhe. Dkt. Pius Chaya (kushoto) akifafanua jambo kuhusu miradi ya elimu alipomtembelea Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Dkt. Erasmus Kipesha ofisini kwake Jijini Dodoma.*

# TEA NA EATV ZAFANYA MATEMBEZI KUHAMASISHA KAMPENI YA NAMTHAMINI

Dar es Salaam




*Wadau wa Elimu wakishiriki katika matembezi ya hisani kufanikisha kampeni ya **"Namthamini"** inayoendeshwa kwa pamoja na TEA na EATV inayolenga kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa kike.*

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na Kituo cha utangazaji EATV wameongoza matembezi ya hisani kwa ajili kuhamasisha umma kushiriki katika kampeni ya Namthamini inayolenga kuweka mazingira rafiki kwa wanafunzi wa kike mashuleni.

Matembezi hayo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, tarehe 25 Agosti 2024 yakianzia Makao Makuu ya EATV Mikocheni Dar es Salaam na kupita maeneo ya Bamaga, Sayansi, Makumbusho na Morocco kisha kurejea tena Makao Makuu ya EATV.

Akizungumza katika kampeni hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa TEA, CPA Mwanahamisi Chambega amesema TEA inashiriki kampeni hiyo muhimu kwa vile inaendana na majukumu ya Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao TEA inausimamia.

"Jukumu la Mfuko wa Elimu wa Taifa ni kukusanya raslimali kutoka sehemu mbalimbali kisha kuzitumia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, ndio maana TEA tunashiriki katika kampeni hii inayolenga kuboresha mazingira ya kujifunzia ya wanafunzi wa kike " amesema CPA Chambega.

*Inatoka Uk. 09*

Kaimu Mkurugenzi huyo wa Huduma za Taasisi wa TEA ametumia fursa hiyo kuhamasisha wadau kuchangia kampeni ya Namthamini akiongeza kuwa watapata faida ambazo ni pamoja na Hati ya Utambuzi wa Uchangiaji wa Elimu (Certificate of Educational Appreciation-CEA) kwa mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001.

Pia, mdau anaweza kutumia hati ya CEA kuombea nafuu ya kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mujibu wa Kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 marejeo ya mwaka 2019.

Faida nyingine ni mdau kutangazwa na kutambuliwa kitaifa, ambapo mchangiaji huandikwa katika rejesta ya kudumu ya wachangiaji wa elimu

Awali Balozi wa Kampeni ya Namthamini Bi. Najma Paul alisema kampeni hiyo ambayo imeendeshwa kwa miaka saba na kituo cha utangazaji cha EATV imeweza kufikia Mikoa 20 nchini ambapo wanafunzi elfu 20 wamepatiwa huduma ya Taulo za Kike kwa kipindi cha mwaka mzima.

Katika matembezi hayo wadau wa Mfuko wa Elimu wa Taifa TotalEnergy Marketing Tanzania Ltd na Sayari Safi waliahidi kuchangia taulo za kike na kufunga miundombinu ya kusafishia maji katika baadhi ya shule zitakazonufaika na kampeni ya Namthamini.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus Kipesha na Mkurugenzi Mtendaji wa EATV Bi. Regina Mengi walisaini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) kuendesha kwa pamoja kampeni ya Namthamni katika hafla fupi iliyofanyika Makao Makuu ya EATV Mikocheni, Dar es Salaam tarehe 16 Juni, 2024.

Kupitia kampeni hii, TEA inashirikiana na EATV kuhamasisha uchangiaji wa rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo na upatikanaji wa maji safi na salama ili kuwawezesha wanafunzi wa kike kuwa na hedhi salama.



*Wadau wa Elimu wakishiriki mazoezi ya kunyoosha viungo baada ya matembezi ya hisani kufanikisha kampeni ya "Namthamini" inayoendeshwa kwa pamoja na TEA na EATV inayolenga kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa kike.*

# TEA, SAUT WAZUNGUMZIA MAENDELEO SEKTA YA ELIMU

Dodoma



*Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi (DRMES) wa TEA Masozi Nyirenda akizungumza katika Mkutano baina ya SAUT na TEA uliofanyika katika Makao Makuu ya TEA jijini Dodoma.*

Menejimenti ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi Bw. Masozi Nyirenda Agosti 15, 2024 walikutana na kufanya mazungumzo na makamu Mkuu wa Chuo cha Mtakatifu Agustino (SAUT) cha Jijini Mwanza Balozi Prof. Costa Mahalu katika Ofisi za TEA Jijini Dodoma.

Katika kikao hicho, Balozi Prof. Mahalu aliongozana na Rev. Prof. Emmanuel Wabanhu ambapo walijadiliana mambo mbalimbali kuhusu Maendeleo ya Sekta ya Elimu, pamoja na namna ya kuboresha mahusiano baina ya SAUT na TEA na kushirikiana katika kuongeza ubora wa elimu.

Awali akitoa neno la utambulisho Kaimu Mkurugenzi Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi Bw. Masozi Nyirenda alisema, jukumu kubwa la TEA ni kusimamia Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao dira yake ni kuwa mfuko bora wa elimu wenye hadhi ya kimataifa na unaotatua changamoto za elimu nchini.

Alisisitiza kuwa, dira hiyo itaweza kufikiwa kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika mfuko huo ili kuwa na maendeleo endelevu kwenye sekta ya elimu hapa nchini.

Kwa upande wake Balozi Prof. Mahalu aliipongeza TEA na Menejimenti yake kwa kuwa mdau mkubwa katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kukiri hali hiyo imesaidia kuinua ubora wa elimu katika maeneo mbalimbali hasa kwenye elimu ya juu.

Chuo cha Mtakatifu Agustino (SAUT) ni moja kati ya Taasisi zilizonufaika na miradi mbalimbali ya uboreshaji miundombinu ya Elimu inayotekelezwa na TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa ambayo hulenga kuinua kiwango cha ubora wa elimu na kuongeza upatikanaji wake kwa usawa.

# MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA, GESIBORA WATETA JIJINI DODOMA

Dodoma

Kaimu Meneja Usimamizi wa Miradi ya Elimu kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Bi. Mwafatuma Mohamed Julai 30, 2024 aliongoza kikao na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Gesibora Bw. Baguma Mpenda, kikao kilichofanyika katika ofisi za TEA Jijini Dodoma.

Lengo la kikao hicho lilikuwa ni kutambulisha kampuni ya Gesibora, kuelezea jinsi inavyofanya kazi pamoja na kuona namna gani kampuni hiyo inaweza kushirikiana na TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa.

Awali akiitambulisha Kampuni ya Gesibora Baguma alisema, kampuni hiyo inajihusisha na ufungaji wa mitambo na usambazaji wa gesi kwa matumizi ya kupikia majumbani, mashuleni, maofisini na hata kwenye hoteli kupitia mfumo maalum ambao umetengenezwa kutunza taarifa za wateja na watumiaji wa gesi.

Bw. Baguma alibainisha kuwa kampuni ya Gesibora ina mpango wa kusaidia kufunga mitambo na kusambaza gesi katika shule za msingi na sekondari ili kuweka mazingira safi na kuwapunguzia wanafunzi na walimu adha ya kutafuta kuni ama mkaa kwa ajili ya kupika.

Kwa upande wake Kaimu Meneja Usimamizi wa Miradi ya Elimu Bi. Mwafatuma Mohamed alieleza kwamba, programu hiyo ya gesibora imewasilishwa wakati muafaka wakati Tanzania na Dunia nzima wako kwenye ajenda ya matumizi ya nishati safi pamoja na utunzaji wa mazingira hatua ambayo itakuwa na manufaa hata kwa sekta ya elimu.



*Kaimu Meneja Usimamizi wa Miradi ya Elimu Bi. Mwafatma Mohamed (kushoto) pamoja na maafisa wengine wakimsikiliza  mdau kutoka kampuni ya GesiBora Bw. Baguma Mpenda (kulia).*

MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA

Tufuatilie Kupitia Mitandao Yetu Ili Kupata Taarifa Zaidi


officialteatz

officialtea_tz

www.tea.or.tz

info@tea.or.tz